


# MAHUSIANO YETU TANO (5) NA MUNGU:

# UHUSIANO WETU WA PILI; "MTUMISHI/MTUMWA KWA BWANA WAKE"

Hujambo!  Nakusalimu asubuhi ya leo.

Katika Chapisho letu la 11 tulizungumza kuhusu uhusiano wetu wa kimsingi na Mungu: yeye kuwa Muumba wetu na sisi tukiwa viumbe wake. Hata hivyo, uhusiano huo wa kimsingi pekee hautoshi. Ingawa tunaishi kama 'viumbe' chini ya neema yake ya jumla (**MATHAYO 5:45**), sio rahisi kumjua Mungu na kwa hakika hatuwezi kutimiza hatima yetu iliyoundwa na Mungu katika uumbaji wake.

Ukweli wa kutisha ni kwamba hakuna kitu ambacho tunaweza kufanya ili kuwa zaidi ya hali ya kuwa 'viumbe' - hakuna chochote tunaweza kufanya ili kumjua Mungu - hakuna tunachoweza kufanya ili kuukuza uhusian wetu na Mungu.

Hapana, sisi ni wanyonge kama viumbe walioanguka - tunamtegemea Mungu kuingilia kati katika maisha ya kila mmoja wetu. Hii ni kwa maana Mungu asipochagua kutuinua kutoka katika hali yetu ya kuanguka, tumehukumiwa.

Lakini kwa bahati nzuri, Mungu aliamua  kufanya hivyo kupitia katika Mwana wake Kristo Yesu:

**WARUMI 5:6-8**; '[6] *Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu.* [7] *Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema.* [8] *Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi*.'

Msalabani, Yesu alizichukua ndani yake dhambi zote za ulimwengu - dhambi zako zote - dhambi zangu zote:

**2 WAKORINTHO 5:21;** *'Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.'*

Mwana wa Mungu alikuja na kufa msalabani SIO kutufanya watu bora, bali kutuua! Alifanya hivyo kwa kuiangamiza asili yetu ya zamani iliyoanguka na kutugeuza kuwa watu wapya kabisa, na kutupa ya asili viumbe wake:

**2 WAKORINTHO 5:17-18;** '[17] *Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.* [18] *Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho*; ‘

Kristo amezifuta dhambi zetu, pamoja na hatia na aibu ya dhambi hizo. Ameivunja laana ya Sheria. Ameshinda Mauti. Haya yote ameyafanya kwa ajili ya viumbe wake wapya, anapoendelea kutimiza Nia Yake Kuu ya kujitengenezea Watu wa kipekee wanaoitwa kwa Jina lake.

Kwa hivyo, ninawezaje kuwa kiumbe kipya? Je, nitaiepukaje hali yangu iliyoanguka ili kuwa sehemu ya utendaji ya Watu hawa wa kipekee wa Mungu?

Hatua ya kwanza ni kukiri kwamba 'mimi ni mwenye dhambi aliyeanguka ninayestahili Jehanamu.' Kwamba 'siwezi kufanya chochote kujirekebisha au kuiepuka hatima yangu iliyoanguka.’

'Ninajitupa kwenye rehema za Mungu na kumkaribisha Yesu kupitia Roho wake Mtakatifu aje moyoni mwangu. Ninakataa maisha yangu ya zamani na ubinafsi wake - pamoja na tamaa yake ya macho - na tamaa yake ya mwili - pamoja na kiburi chake cha uzima. Ninasalimisha dhamira na mapenzi yangu kuwa dhamira na mapenzi ya Baba.’

'Roho wake anaponibadilisha na kukaa ndani yangu, ninaweka mtazamo wangu katika kugeuzwa kuwa mfano na sura ya Yesu - kumjua na kumwabudu na kumpenda Yesu - kumtii na kumtumikia na kumwakilisha Yesu - kumfurahia Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu sasa na hata milele.'

Majabali na mabingwa wa kiroho wa zamani walichukua hatua hii ya kwanza. Na kwa sababu walifanya hivyo, waliweza kujitambulisha pamoja na Yesu Kristo kama watumwa wake;

- "*Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu*…" **Warumi 1:1**
- "*Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo*…" **2 Petro 1:1**
- "*Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo*…" **Yakobo 1:1**
- "*Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo*…" **Yuda 1:1**
- "*Ufunuo kutoka kwa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu ili kuwaonyesha watumwa wake ni nini lazima litendeke upesi... kwa kumtuma malaika wake kwa mtumwa wake Yohana*." **Ufunuo 1:1**

Sisi sote tunataka kuwa huru. Hakuna hata mmoja wetu anayetaka kumilikiwa kama mtumwa na mtu mwingine. Lakini la kushangaza ni kwamba, njia ya kuuelekea uhuru ulio wa kweli ni kuwa mtumwa ama mtumishi wa Yesu Kristo kwanza.

**Wagalatia 5:1** "*Ni kwa ajili ya uhuru ambao Kristo ametuweka huru*."

Walakini sio nia ya Mungu kwamba tuwe watumwa mfano wa watu wa Afrika Mashariki, ambao Waislamu wafanya biashara ya utumwa waliwauza katika utumwa wa Ghuba ya Uajemi. Hapana, hapa tunazungumzia kitu tofauti sana.

Katika Kumbukumbu la Torati utumwa huu umefafanuliwa:

**Kumbukumbu La Torati 15:12-17;** '[12] *Ikiwa nduguyo, mume wa Kiebrania, au mwanamke wa Kiebrania, akiuzwa kwako, naye amekutumikia miaka sita; basi mwaka wa saba mwache huru aondoke kwako.* [13] *Nawe utakapomwacha huru aondoke kwako, usimwache aende zake mikono mitupu;* [14] *umwangalie kwa wema katika kundi lako, na sakafu yako ya nafaka, na kinu chako cha divai; mpe kama alivyokubarikia BWANA, Mungu wako.* [15] *Nawe kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri, akakukomboa BWANA, Mungu wako; kwa hiyo mimi nakuamuru neno hili hivi leo.* [16] *Hata itakuwa, akikuambia, Siondoki kwako; kwa sababu akupenda wewe na nyumba yako, kwa kuwa yu hali njema kwako;* [17] *ndipo utwae uma, uupenyeze katika sikio lake uingie katika ubao wa mlango, naye atakuwa mtumishi wako milele. Na kijakazi chako naye mfanye vivyo*.'

Mtu aliyefilisika alijiuza katika utumishi ili aweze kuyalipa madeni yake. Baada ya miaka sita, deni lake kwa aliyemlipia lilifutwa na ilibidi aachiliwe na kuwekwa katika utunzaji wa nyumba yake mwenyewe.

Katika kipindi hicho, ikiwa mtu huyo angejionyesha kuwa sehemu ya thamani ya nyumba ya bwana wake - yaani kuwa kama mmoja wa familia ya bwana zaidi ya kuwa mtumwa - angeweza kuchagua kukaa na kudumu katika nyumba ya bwana wake. Angeweza kuwa sehemu ya nyumba ya bwana wake bila kuwa 'mtumwa' tena. Hii ni kwa kuwa alitaka kuwa sehemu ya nyumba ya bwana wake milele.

Alipelekwa mpaka kwenye mwimo wa mlango wa nyumba na upanga ukatobolewa masikioni mwake, kumaanisha kwamba alikuwa ameshikanishwa milele pamoja na nyumba hiyo ya bwana wake. Baada ya uamuzi huo, bwana wake alichukua jukumu la kudumu la kumtunza. 'Mtumwa' huyo sasa naye aliahidi kutoa huduma ya uaminifu kwa bwana wake milele.

Unaelewa?

Je, umeyatoa maisha yako kwa Yesu? Je, unaweza kusema pamoja na Paulo;

**WAKOLOSAI 3:4** '*Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu*.'

Je, umekufa katika asili yako iliyoanguka? Je, umezaliwa mara ya pili? Je, umebatizwa katika nyumba ya Mungu? Je, umejazwa na Roho wa Yesu? Je, umejitolea bila shauku kutumika katika radhi ya Mfalme wa milele?

Mwanzo wa maisha ya kweli, mwanzo wa uhuru wa kweli, mwanzo wa mbingu ya milele, kifo cha uharibifu wako, ubinafsi wako, na ubatili wako ni kuingia katika furaha ya utiifu ya Yule aliyekuumba na anayekupenda, sasa na hata milele.

Kama Mungu alitutolea uhusiano huu naye, tungeanguka kifudifudi kwa shukrani
kwa kuwa ameturuhusu sisi kuishi katika nyumba yake na kumtumikia milele. (ZABURI 23:6 ).

Lakini kuna zaidi. Mengi, mengi zaidi. Nitakwambia juma lijalo.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.

Ni wako Douglas Douglas Van Devender. Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.